

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI

Simu: +255-26-2323201-7
Nukushi: +255-26-2323208
Barua pepe: nje@nje.go.tz
Tovuti: www.foreign.go.tz



Mji wa Serikali,
Mtumba,
S.L.P 2933,
40466 DODOMA

Unapojibu tafadhali taja:

Kumb. Na: QA 298/485/01

14 Septemba, 2022

Waheshimiwa Mabalazi,

Balozi za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

**Yah: HUDUMA ZA BENKI YA STANBIC TANZANIA NA BIDHAA
KWA AJILI YA DIASPORA**

Tafadhali husika na somo tajwa hapo juu.

2. Wizara inapenda kuwafahamisha kuwa tumepokea barua kutoka Benki ya STANBIC Tanzania ikituarifu kuhusu huduma na bidhaa za Benki hiyo na utayari wao kufikisha huduma zao kwa Wafanyakazi wa Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki watakaozihitaji, waliopo Makao Makuu ya Wizara na katika Balozi za Tanzania nje ya nchi. Benki hiyo imejipanga kufikisha taarifa za huduma zao kwa Wafanyakazi wote Ubalozini kupitia *Webinar Sessions*, kama ilivyoanishwa hapa chini;

➤ Ulaya	26 Septemba, 2022
➤ Marekani	27 Septemba, 2022
➤ Umoja wa Falme za Kiarabu	28 Septemba, 2022
➤ Nchi za Afrika	29 Septemba, 2022
➤ China na nchi nyingine za Asia	30 Septemba, 2022

3. Kwa ufafanuzi na maelezo zaidi kuhusu huduma hizo na nyingine zinazotolewa na Benki ya STANBIC Tanzania, Wizara inawasilisha kwenu mawasiliano ya **Bi. Edditrice Marco – Mkuu wa Kitengo cha Wateja Maalum, Simu namba +255 767 210 975** na **Barua pepe: Edditrice.marco@stanbic.co.tz** Aidha, Watumishi wa Benki hiyo watawatafuta katika tarehe zilizoanishwa hapo juu na Wizara inaomba wapewe ushirikiano.

Tunashukuru kwa ushirikiano.

Balozi James G. Bwana
Kny: **KATIBU MKUU**

Nakala: Mkurugenzi wa Wateja Binafsi,
Benki ya Stanbic Tanzania,
S.L.P 72647,
DAR ES SALAAM.